**JAMHURIYA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA Ufunguzi wa Tamasha la 41 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni

**BAGAMOYO**
**11 NOVEMBA, 2022**

- ***Mheshimiwa Mohammed Omar Mchengerwa (Mb), Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo;***
- ***Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote mliopo;***
- ***Mheshimiwa Abubakar Kunenge, Mkuu wa Mkoa wa Pwani;***
- ***Dkt. Hassan Abbasi, Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo;***
- ***Makatibu Wakuu na Naibu Katibu Mkuu mliopo;***
- ***Zuena Omar, Katibu Tawala Mkoa wa Pwani;***
- ***Waheshimiwa Mabalozi wa Nchi Mbalimbali mliohudhuria hapa;***
- ***Mhe. Zainabu Abdallah Issa, Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo,***
- ***Mhe. Dkt. Muharami Mkenge, Mbunge, Jimbo la Bagamoyo,***
- ***Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo;***
- ***Viongozi wa Chama na Serikali mliopo;***
- ***Viongozi wetu wa Dini, Kamati ya Amani;***
- ***Wadhamini wa tamasha na Kamati ya maandalizi ikiongozwa na Mwenyekiti wake;***
- ***Wakurugenzi na Wakuu wa Taasisi za Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo;***
- ***Marais wote wa Mashirikisho ya Sanaa Tanzania;***
- ***Ndugu waandishi wa habari;***
- ***Wasanii wote (ndani na nje ya Tanzania), Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana.***

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania…**

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia uhai na kutuwezesha kuwa mahali hapa siku hii ya leo. Napenda kukushukuru kwa dhati Mheshimiwa Waziri Mchengerwa kwa kunialika kuwa Mgeni Rasmi katika hafla hii muhimu ya ufunguzi wa Tamasha la 41 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni.

Nikiri tu kuwa nimekuwa nikilisikia Tamasha hili kwa miaka mingi na leo ninayo furaha kuwa sehemu ya tukio hili muhimu.

Aidha, nakupongeza wewe Mheshimiwa Waziri, uongozi na watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake, Kamati ya Maandalizi na wenyeji wetu hapa Bagamoyo wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa Bw. Kunenge na Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Zainab Abdallah kwa maandalizi mazuri ya Tamasha hili ambalo kwa kweli limefana sana. **Hongereni sana!**

Vilevile kwa namna ya kipekee kabisa napenda kuipongeza Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) kwa kuendelea kuwa wabunifu na kutoa elimu ya sanaa, kutangaza sanaa na utamaduni pamoja na kufundisha maadili ya Sanaa kwa vijana wetu hapa nchini. Serikali inathamini mchango wenu mkubwa katika kuhakikisha Sanaa na utamaduni wetu unatambulishwa kwa weledi. **Tunawashukuru na kuwapongeza sana!**

Napenda nitumie nafasi hii pia kuwakaribisha wageni wote kutoka ndani na nje ya nchi. Nimefurahi sana kuona mwitikio mkubwa wa wananchi na wadau wengi kushiriki katika Tamasha hili. Hii inadhihirisha kukubalika na kukua kwa Tamasha hili hapa nchini na kimataifa. Kwa maandalizi haya niliyoyaona naamini mtafurahia na kujifunza mengi kuhusu Sanaa na Utamaduni wetu.

***Ndugu viongozi, wageni waalikwa, mabibi na mabwana.***

Katika uhai wake, Baba wa Taifa Hayati Julius Kambarage Nyerere, aliwahi kusema kuwa ***"…sanaa ndiyo roho ya maisha ya taifa lolote. Nchi isiyo na Sanaa yake ya asili ni mkusanyiko wa watu tu usio na roho."*** Taifa letu lenye zaidi ya makabila 120 linaunganishwa na Sanaa na Utamaduni wake wa asili ambao tunaweza kuuelezea pia kupitia lugha yetu adhimu ya Kiswahili. Sanaa na utamaduni wetu ndiyo roho inayotuunganisha na kututambulisha popote duniani kama taifa la Tanzania.

Leo tunapoadhimisha Tamasha la 41 la kimataifa la sanaa na utamaduni naomba nirejee tena hotuba ya Mwalimu Nyerere wakati akianzisha Wizara hii ambapo alisema "***Nimeanzisha Wizara hii ili isaidie kufufua Fahari yetu katika mambo yetu ya asili. Ningependa itafute mambo yetu yanayofaa kutoka katika kila kabila na ifanye mambo hayo kuwa ni mambo ya taifa zima la Tanganyika***" mwisho wa kunukuu. Nimefurahi kuona Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo mmeendelea kutekeleza maelekezo haya kupitia Tamasha hili. Kwa kweli nimeburudishwa sana na vikundi vya ngoma na sanaa

zetu za asili kutoka katika makabila mbalimbali ya Tanzania. **Hongereni sana!** Aidha, nawapongeza Wizara kwa kurejesha wiki ya utamaduni na kwa kufanya maadhimisho ya siku ya Kiswahili duniani ambayo yalifana sana.

***Ndugu viongozi, wageni waalikwa, mabibi na mabwana.***

Wizara na Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) imefanya uamuzi sahihi kulifanya Tamasha hili kuwa la kimataifa. Uamuzi huu umesaidia kutambulisha Sanaa na utamaduni wetu katika mataifa mengine, kuitangaza nchi yetu, kuvutia wageni na hivyo kuendelea kuunga mkono jitihada za Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuitangaza nchi yetu na vivutio vyake kama alivyotuonesha kwa vitendo kupitia filamu ya **Tanzania: The Royal Tour**.

Aidha, kupitia Tamasha hili, vijana wetu wa Kitanzania wamepata fursa ya kubidhaisha Sanaa zao na kujipatia vipato; kukutana na wasanii mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi na kuweza kujifunza, kubadilishana uzoefu na hata kupata masoko. Ni matumaini yangu kuwa, kupitia Tamasha hili, vijana wengi zaidi wataendelea kuhamasika na kushiriki matamasha na mikutano ya aina hii. Nafahamu pia mwezi huu wa Novemba 2022 mnaratibu kufanyika kwa mkutano mkubwa wa wadau wa sekta ya muziki Afrika yaani "***Music in Africa Conference***" pale Dar es Salaam. Nitumie fursa hii kuwahamasisha wasanii wetu na wadau husika kujiandikisha na kushiriki kikamilifu katika mkutano huu muhimu kwani utakuwa ni fursa nyingine ya kukutana na wadau mbalimbali na kujifunza namna bora ya kuifanya Sanaa yetu ya muziki izidi kusonga mbele.

***Ndugu viongozi, wageni waalikwa, mabibi na mabwana.***

Sekta ya burudani (entertainment industry) kupitia sanaa na utamaduni, ni uchumi. Kulingana na takwimu zilizopo, sekta ya burudani ndiyo sekta iliyokua kwa kasi kuliko sekta zote nchini ikikua kwa asilimia 19 katika mwaka 2021. Aidha, Sekta hii inaajiri vijana wengi na inaweza kutengeneza matajiri wengi endapo vipaji vya wasanii wetu vitaendelezwa. Vilevile, sekta hii inasaidia sana katika kuitangaza nchi yetu na lugha yetu adhimu ya Kiswahili kupitia kazi za wasanii mbalimbali. Napenda kuwapongeza vijana wetu kama "The Ramadhan Brothers" na wengine wengi ambao wameweza kutumia sekta hii kuitangaza nchi yetu na pia kujikwamua kiuchumi.

Kupitia hadhara hii, napenda kuwahakikishia kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Samia itaendelea kuunga mkono wasanii hapa nchini na kuzipa kipaumbele sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo ili ziweze kufaidisha vijana wengi zaidi. Na hii ndio sababu, kutokana na umuhimu, Mheshimiwa Rais aliamua kuiondoa sekta ya Habari kutoka sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo ili kutoa nafasi kwa Wizara kutekeleza wajibu wake kwa ufanisi zaidi. Naamini kutokana na mabadiliko yaliyofanyika na yanayoendelea kufanyika, vijana wetu wamepata nguvu, motisha na ari mpya kufika mbali na kufanikiwa zaidi kupitia sekta hizi za utamaduni, Sanaa na Michezo.

Kupitia jukwaa hili ninapenda kuzipongeza timu zetu za Tembo Warriors na Serengeti Girls kwa kufuzu kwa mara ya kwanza kushiriki michuano ya Kombe la Dunia kwa mpira wa miguu ambapo zilifikia ngazi ya robo fainali. Mafanikio yenu yalitoa motisha kwa serikali kuendelea kuboresha mazingira na kuimarisha sekta hizi ili zije kuwa kati ya sekta muhimu zenye kuleta chachu ya maendeleo ya nchi na pia kuinua vijana wetu kiuchumi.

***Ndugu viongozi, wageni waalikwa, mabibi na mabwana.***

Kama nilivyosema hapo awali, Sanaa ndiyo roho ya taifa lolote. Hivyo hatuna budi kuhakikisha inakuwa yenye asili na maadili yanayotuwakilisha sisi kama Watanzania. Naomba kuwasihi watanzania, hususan wasanii wetu wa kizazi kipya, kuepuka kuiga kila tamaduni bila kuchuja wala kuzingatia maadili yetu. Na endapo italazimika kuiga Sanaa na tamaduni za mataifa mengine, basi tuhakikishe tunaiga zile zinazoendana na maadili na tamaduni zetu ili tusipoteze asili, heshima na utambulisho wetu. Tunaweza kuiga yale mazuri tunayoyaona yanatufaa na yanaendana na maadili yetu, lakini yale yasiyotufaa tuwaachie wenye tamaduni zao. Kwenye hili naomba pia nitoe rai kwa wasanii wa muziki na filamu kuhakikisha mnazingatia maadili na miongozo ya Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) pamoja na Bodi ya Filamu Tanzania mnapotengeneza maudhui ya kazi zenu. Kumbukeni kuwa ninyi ni kioo cha jamii na pia mkitengeneza taswira mbaya kupitia kazi zenu mtasababisha jamii kutoheshimu kazi yenu. Hali kadhalika, mkitengeneza taswira nzuri, wazazi na walezi wengi hatutakuwa wagumu kuruhusu vijana wetu kujihusisha na Sanaa kupitia muziki au filamu.

***Ndugu viongozi, wageni waalikwa, mabibi na mabwana***

Serikali inaendelea na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025 ambayo inatoa muongozo mzuri sana wa masuala yanayopaswa kutekelezwa ili kuiendeleza sekta ya Utamaduni, Sanaa na

michezo. Yapo mambo ambayo utekelezaji wake umeanza, ikiwa ni pamoja na kufanya Matamasha kama haya; kuongeza wigo wa matumizi ya lugha ya Kiswahili; kubainisha maeneo yenye historia muhimu kuwa vivutio vya utalii; kuimarisha TaSUBa ili kuboresha tasnia ya Sanaa; kulinda kazi za wasanii kupitia utaratibu wa Stempu; kuhifadhi kidijitali nyaraka mbalimbali kuhusu historia ya Ukombozi wa Bara la Afrika ambapo taifa letu lilikuwa kiungo muhimu sana; pamoja na kuimarishwa kwa michezo ya shule za msingi na sekondari, UMITASHUMTA na UMISSETA. Napenda kutumia fursa hii kuielekeza Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kufanya tathmini ya hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa maelekezo yote ya Ilani ya CCM na kuhakikisha yanatekelezwa kwa ukamilifu.

***Ndugu viongozi, wageni waalikwa, mabibi na mabwana***

Kabla sijahitimisha hotuba yangu napenda kutoa maelekezo yafuatayo:

**Kwanza**, Wizara iendelee kuzisimamia sekta hizi kikamilifu ili ziendelee kuwa na mchango thabiti katika uchumi wa nchi yetu;

**Pili**, Shughuli za michezo na Sanaa ziendelee kusimamiwa vyema mashuleni kwa sababu sasa tunazitambua kama taaluma na ajira rasmi;

**Tatu**, Viongozi katika mamlaka zote za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa waendelee kushirikiana na Wizara katika kuendeleza shughuli za utamaduni, Sanaa na michezo ikiwemo kuyalinda maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli hizi;

**Nne**, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ishirikiane na Wizara ya Maliasili na Utalii kuhifadhi, kutunza na kutangaza tamaduni za makabila kupitia utalii wa kiutamaduni (*cultural tourism*) na kutoa nafasi kwa makabila yetu hapa nchini kuonesha tamaduni zake kwenye chakula, dawa za asili, mavazi, makazi pamoja na aina ya ngoma na burudani zake. Aidha, naagiza kila mkoa kuweka utaratibu wake wa kuendeleza utamaduni wa mkoa huo kama sehemu ya utalii wa kiutamaduni;

**Tano,** Kama alivyoelekeza Mheshimiwa Rais wakati alipowaita Ikulu Serengeti Girls, Julai mwaka huu, Wizara hii ya Utamaduni na ya Fedha ziendelee kujadiliana juu ya namna bora ya kuongeza Bajeti ya Wizara ili zile shughuli muhimu zitakazochagiza ukuaji wa uchumi na ajira kwa vijana kupitia sekta hizi za burudani zisikwame. Na kwenye hili

Mheshimiwa Waziri nitaomba ripoti suala hili limefikia wapi kiutekelezaji ifikapo Desemba 30 kabla ya kufunga nusu mwaka wa fedha;

**Sita,** Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo mshirikiane na wadau husika kuendelea kutoa elimu na kutafuta namna bora ya kutatua changamoto zote zinazohusiana na hakimiliki, hakishiriki, mirabaha na mikataba katika sekta ya Utamaduni na Sanaa kwa ujumla;

**Saba**, Tamasha hili la Bagamoyo liendelee kuboreshwa kila mwaka ili lifikie hadhi ya matamasha mengine makubwa duniani;

**Nane**, Wizara itoe kipaumbele kwenye kuendelea kukitangaza Kiswahili duniani; kuanzisha Kituo cha Taifa cha Sanaa cha Watoto na Vijana wenye vipaji ambao hawapo kwenye mfumo rasmi wa elimu; kuanza ujenzi wa Jumba Changamani la Uzalishaji wa Filamu; na pia kuanzisha shule maalum za kukuza vipaji vya wanamichezo (sports academy);

**Mwisho,** Pamoja na maboresho yaliyofanyika, Tamasha liendelee kuzingatia masuala ya Muungano ikiwemo kuhakikisha vikundi na Sanaa nyingine zaidi kutoka Zanzibar zinapata nafasi katika Tamasha hili.

Naamini mkitekeleza haya, tutapiga hatua kubwa sana katika kutangaza na kubidhaisha Sanaa na Utamaduni wetu pamoja na kukuza sekta ya michezo nchini.

***Ndugu viongozi, wageni waalikwa, mabibi na mabwana***

Napenda nihitimishe hotuba yangu kwa kuwashukuru kila mmoja aliyetimiza wajibu wake kufanikisha tamasha hili. Lakini kipekee kabisa, napenda kuwashukuru wadhamini wetu waliotuunga mkono ikiwa ni pamoja na BASATA, Shirika la Bima la Taifa (NIC), CRDB Bank, Taasisi ya AfroFest kutoka Canada, Heineken, pamoja na wengine wote. **Asanteni sana!**

Baada ya kusema hayo, naomba kutamka kuwa Tamasha la 41 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo limezinduliwa rasmi.

**Wasanii oyee…**

**Asanteni sana kwa kunisikiliza**